East African Journal of Swahili Studies, Volume 5, Issue 1, 2022
Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.803

**East African Journal of Swahili Studies**
eajss.eanso.org
**Volume 5, Issue 1, 2022**
**Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475**
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Ufungamanisho wa Fonolojiya Othografiya na Teknolojiya katika Kukiyand̪ika Upya Kiswahili Sanifu; Kujiokowa na Kuokowa Mustakabali wa Lahaja-Dadaze[1]

*Dr. Mohamed Karama, PhD*[1*]

[1] Chuo Kikuu cha Kabianga, S. L. P. 2030 – 20200, Kericho, Kenya.
[*] ORCID ID: https://orcid.org/0000-0003-2341-9966; Barua pepe ya mawasiliano: mkarama@kabianga.ac.ke

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.803**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*24 Agosti 2022*

**Istilahi Muhimu**:

*KiSwahili, Fonolojiya, Usanifishaji, Othografiya, Teknolojiya, Jumuiya ya Afrika Mashariki*

**IKISIRI**

Lahaja za kiAmu, kiMvit̪a zafa, na lahaja nyenginezo za kiSwahili yasemekana zishakufa. Makala haya yanaonesha kuwa usuli wa matatizo haya ni mapungufu ya juhud̪i za kukisanifisha kiSwahili wakat̪i wa ukoloni. Vigezo va uwamilifu wa kut̪afaut̪isha maana, na kiwango cha matumizi wa saut̪i hiyo katika lugha, ni mambo yaliyopuuzwa na Kamati ya Lugha kwa sababu ya kut̪afut̪a unafuu wa kusanifisha. Tukifuwatʰa nadhariya-tʰetʰe ya Kina cha Othografiya, saut̪i hizi amilifu tumeziyonesha kuwa zachʰangiya katika kusoma maand̪ishi yaliyoand̪ikwa kwa sababu kiSwahili ni lugha yenye othografiya ya maonroni, yaani, kuna mnasaba wa moja kwa moja kati ya saut̪i na kiwakilishi chake kihati; kitamkwavo nrivo kiyand̪ikwavo. Kwengezeya, mfumuko wa TEKNOHAMA umeipa t̪ena, lugha ya kiSwahili, nafasi ya kufaid̪ika na saut̪i hizi kwa kutiya kila kʰitʰu katika nukt̪a ya kimahesabu hivo kurahisisha utambuzi wa saut̪i hizi na urahisi wa kuzitumiya katika masomi ya shuleni na kwenye t̪afsiri mashine ya makala ya kiSwahili. Ikawa nat̪ija ipatikanayo ni kukiokowa kiSanifu kut̪okana na kuziokowa lahaja dada zake. Lakini zaid̪i, ni kupatikana ut̪angamano wa lugha zot̪ʰe nchini Kenya na utambulisho muwafaka katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**APA CITATION**

Karama, M. (2022). Ufungamanisho wa Fonolojiya Othografiya na Teknolojiya katika Kukiyand̪ika Upya Kiswahili Sanifu; Kujiokowa na Kuokowa Mustakabali wa Lahaja-Dadaze. *East African Journal of Swahili Studies*, *5*(1), 259-272. https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.803.

[1] Nawat̪abarukiya makala haya Dkt. Paul M. Musau na Dkt. Mwanakombo N. Mohamed, wot̪ʰe marehemu, kwa kunijuza mengi katika t̪aalimu.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.803

**CHICAGO CITATION**

Karama, Mohamed. 2022. “Ufungamanishowa Fonolojiya Othografiyana Teknolojiyakatika Kukiyand̪ika Upya Kiswahili Sanifu; Kujiokowana Kuokowa Mustakabali wa Lahaja-Dadaze”. *East African Journal of Swahili Studies* 5 (1), 259-272. https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.803.

**HARVARD CITATION**

Karama, M. (2022) “Ufungamanishowa Fonolojiya Othografiyana Teknolojiyakatika Kukiyand̪ika Upya Kiswahili Sanifu; Kujiokowana Kuokowa Mustakabali wa Lahaja-Dadaze”, *East African Journal of Swahili Studies*, 5(1), pp. 259-272. doi: 10.37284/jammk.5.1.803.

**IEEE CITATION**

M. Karama, “Ufungamanishowa Fonolojiya Othografiyana Teknolojiyakatika Kukiyand̪ika Upya Kiswahili Sanifu; Kujiokowana Kuokowa Mustakabali wa Lahaja-Dadaze”, *EAJSS*, vol. 5, no. 1, pp. 259-272, Aug. 2022.

**MLA CITATION**

Karama, Mohamed. “Ufungamanishowa Fonolojiya Othografiyana Teknolojiyakatika Kukiyand̪ika Upya Kiswahili Sanifu; Kujiokowana Kuokowa Mustakabali wa Lahaja-Dadaze”. *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 5, no. 1, Aug. 2022, pp. 259-272, doi:10.37284/jammk.5.1.803.

## UTANGULIZI

Yasemekana kiMvit̪a na kiAmu ni lahaja mbili zilidhoofika katika matumizi ya kawaid̪a hivi kwamba zimo katika sakarat̪il maut̪i – zimo katika hat̪ari ya kufa – na pengine lahaja nyenginezo za kiSwahili yaweza kuwa zishakufa t̪ayari. Ut̪afit̪i wa Karanja (2012) umechora picha hiyo ya ‘kuhuzunisha’ kuhusu hali ya lahaja hizi mbili ilivo hivi sasa nchini Kenya. Katika hit̪imisho lake, Karanja anat̪ahadharisha kwamba kufa kwa lahaja hizi ni hasara kwa kiSwahili sanifu (soma kiSanifu) kwani huzit̪egemeya lahaja hizi kwa makuzi yake. Kwengezeya t̪ʰafit̪i za Mazrui (1981), Githinji na Njoroge (2017) na Mazrui na Chimerah (2019), zinaonesha kuwa miyelekeo ya watumiyaji wa lahaja ya kiMvit̪a – piya lahaja nyenginezo – inaenreleya kukipend̪eleya kiSanifu katika mawand̪a mengi mbali ya mashuleni na makazini. Bila kuiza, wimbi la kiSanifu lishaanza kutʰeka lahaja kwa mkupuwo mmoja na yaonekana, kama wasemavo Mazrui na Chimerah, kuna kijilugha chengine – kipwara (mchanganyiko wa kipwani na kibara na kiSanifu) – chajichipuza. Crystal (2003), na wat̪afit̪i wot̪ʰe tuliyotaja awali, wameonesha kuwa ikiwa lugha it̪akosa kutumiwa kabisa na wenyeji; isipitishwe kut̪oka wazee kwenra kwa kizazi kinachokuja; na mawanda yake ya matumizi yapunguwe kwa kiyasi kikubwa, basi lugha hiyo imo hat̪arini kuangamiya na ni jambo linalotiya moyo huzuni – ni kama kuonrokewa na mtu wa karibu nawe. Hat̪a hivo, t̪ʰafit̪i tulizozitaja, vigezo vake va ut̪afiti na mahit̪imisho yao, yameegemeya zaidi masiala ya kiisimujamii (mawand̪a ya matumizi na miyelekeo ya wasemaji) lakini makala haya yat̪aegemeya zaidi kwenye manahaji ya kifonolojiya ambayo ikifuwatʰwa basi lahaja zot̪ʰe za kiSwahili (kiSanifu na kiAsiliya) zit̪aokoka.

Uwand̪a wa t̪aaluma ya fonolojiya huangaziya uwamilifu wa kipanre cha saut̪i ama ziyad̪a saut̪i katika kuwasilisha maana it̪arajiwayo katika mtʰongoo au kauli. Sifa bainifu ya lahaja za kiSwahili za Kenya dhid̪i ya kiSanifu ni saut̪i za menoni (Bakari, 1985). Saut̪i hizo huwa na uwamilifu wa kuweza kut̪afaut̪isha na kubadilisha maana wakat̪i zinapotumika katika maneno kama alivobainisha Shariff (1988). Katika isimu-jumla, kipashiyo cha fonimu nricho kibad̪ilishi kinachot̪afit̪iwa na huangaziwa kimahesabu katika lugha ya kawaid̪a ya wanenaji wa lahaja fulani (Chambers & Trudgill, 2004) na hivo kubainisha sifa zinazot̪afaut̪isha lahaja moja na nyengine. Ni t̪afaut̪i na t̪ʰafit̪i za kiisimujamii ambazo hutiliya maswala ya nje ya isimu halisi: d̪ini, siyasa, t̪abaka, uhasama kama alivofafanuwa Mkude (2010).

Tulifanya ut̪afit̪i wa kimakt̪aba na kutiliwa nguvu na t̪ajiriba ya mwandishi wa makala haya, na uchanganuzi wetʰu ni wa kimaelezo. Mwand̪ishi wa makala haya ni mzawa, mkaaji, na mfanyikazi katika sehemu zinazozungumzwa lahaja ya kiMvit̪a na amebahat̪ika kusoma isimu ya kiSwahili mpaka chuwo kikʰuu, hivo ana ujuzi angalau wa kuzipambanua saut̪i, mifumo yake, na maana za maneno ya lahaja hiyo. Mchʰango huu wa wazawa-wasomi wa lahaja hizi umepawa nguvu na Bakari (1985) kwa kut̪owa ufunuwo mwingi kuhusu mifanyiko ya kiisimu nrani ya lahaja hizi. Isit̪oshe, ut̪afit̪i wa Hayward na we. (1989) umekubalika japo

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.803

Maalim Yahya ṯu nriye msailiwa. Tukiyengezeya wa Sivertsen, akinukuliwa na Chambers na Trudgill (2004, uk. 46), amefanya uṯafiṯi wake wa *Cockney Phonology* kwa wasailiwa watʰu-wazima wane ṯu.

Makala haya yaṯajikita katika kwelezeya zaidi lahaja ya kiMviṯa ambayo nriyo iliyomo haṯarini kwa 'uvamizi' wa kiIngereza, kiSanifu, na Sheng, kama ilivojiṯokeza katika ṯʰafiṯi tulizozitaja hapo awali, na kuṯowa mifano zaiḏi kuṯoka lahaja nyengine iṯakapohiṯajika. Madhumuni yetʰu yamekuwa kwangaziya juhuḏi mbalimbali zilizofanywa kuziyeleza sauṯi za lahaja za kiSwahili na kuzibuniya othografiya zake; kuṯathmini matumizi ya kigezo cha kifonolojiya katika kutambuwa na kweleza maana za maneno kuṯokana na othografiya; na kuchanganuwa umuhimu wa teknolojiya katika kuzitumisha na kuzihuwisha lahaja hizi kwa manufaa ya wanafunzi wa kiSanifu katika zama hizi za nukṯa. Katika makala haya 'kiAsiliya' iṯarejeleya kiSwahili cha lahaja-msingi kumfuwata Mazrui (1981) na 'kiSanifu' iṯarejeleya kiSwahili sanifu. Isṯilahi 'othografiya' iṯatumika sawiya na 'mwanḏiko' au 'hati'. Aidhan, neno 'sauṯi' liṯarejeleya isṯilahi 'fonimu' piya.

Azma ya ṯʰafiṯi za Karanja, Githinji na Njoroge, na Mazrui tulizotaja awali ilikuwa kufafanuwa miyelekeo na matumizi ya kiSanifu dhiḏi ya kiAsiliya na moja ya kifaa cha kupata data kilikuwa ni kutumiya hojaji; kifaa hicho kiliṯosheleza uhiṯaji wao. Kulingana na maelezo ya Chambers na Trudgill (2004) na Milroy na Milroy (1999) wameonesha njiya muwafaka ya kupata data ya isimu-jumla ni kupata mazungumzo ya kawaiḏa bila maingiliyano ya jinsi yoyoṯʰe kwa wazungumzaji kuṯoka kwa mṯafiṯi au mazingira waliyomo wazungumzaji. Ijapokuwa hatukufanya ukusanyaji wa data msingi lakini uchanganuzi wetʰu wa data ya upili iṯaṯosheleza kukidhi haja ya maelezo yetʰu na kuṯowa mahiṯimisho juu ya data hiyo.

## KISWAHILI NA KISANIFU NI ISṮILAHI MOJA?

Kwa maoni yetʰu, ni msururu wa viṯabu va kiyaḏa va Massamba na we. kuhusu sarufi ya kiSwahili unaobainisha kwamba wanashughulikiya mahasusi 'kiSwahili sanifu' kazi nyengine za kiisimu huchanganya lugha hizi mbili kumaanisha moja: kiSwahili na kiSanifu, kwa mfano, Karanja (2012), CASAS (2012), Mgullu (1999). Ikawa wakisema kiSwahili nriyo ishajumuisha lahaja zoṯʰe na kiSanifu. Haya nriyo yanayopelekeya wasomi kutatiza kwamba kiSwahili na kiSanifu ni kʰitʰu kimoja, filhali kiSanifu ni moja kati ya lahaja za kiSwahili – ṯena chʰanga ya zoṯʰe (Chiraghdin, 1977). Si ajabu katika kuṯokuṯafauṯisha baina ya lugha hizi mbili kumepelekeya wasomi fulani kusema kwamba kiSwahili ni lugha haina wenyewe (University of Cape Town, 2022; Chimerah, 1999). Tukumbuke kuwa kuna: kiSwahili (lugha), uSwahili (utamaduni), uSwahilini (ardhi ya waSwahili) na waSwahili (kabila) kama ilivofafanuliwa katika kazi za Mazrui (2007), Mbaabu (1985) na Eastman (1994). Katika mazungumzo na Profesa Chimerah (kwa simu 06/06/2022) nilipomuuliza kuhusu yeye kusema kwamba kiSwahili hakina kabila alinijibu kwamba alikuwa anamaanisha kiSanifu. Alinifafanuliya kwamba lugha sanifu ni ya kutengezwa au kubuniwa na waṯaalamu na kupawa wananchi wa sehemu fulani kwa sababu, miyongoni mwazo, za kiuṯawala; jambo analolitaja Mazrui (2007, uk. 5) kwa mukṯadha wa kifasihi. Kuṯafauṯisha ama kuṯoṯafauṯisha kiSwahili kuwa na kabila kwaṯegemeya piya sababu za kisiyasa ya nchi husika (Mazrui, 2007, uk. 4); nchini Kenya linatambulika (Kenya National Bureau of Statistics, 2009, uk. 87).

Kuna kazi kadhaa ambazo zimeeleza kwamba kiSwahili chafaa kisanifishwe. Stigand (1915), Steere (1919), Sacleux (1939) na kabla yao Krapf (1882) wakirejelewa katika Whiteley (1993:80) na za karibuni Chiraghdin(1977), Mazrui (1981), na Massamba na we. (2004). Kazi hizi zaeleza kuhusu lugha ya kiSwahili lakini na kutaja kwamba kuna ṯafauṯi ya kiSwahili na kiSanifu. Mazrui anaonesha kuwa kuna 'lahaja za kimsingi' ambazo hujumuisha lahaja za kiAsiliya (miyongoni mwazo kiVumba, kiMviṯa, kiAmu, kiṮʰikuu) na lahaja za kiupili au kiSanifu. Nriposana, kumeṯokeza waanḏishi wanaoonesha kuwa kuna kiSwahili asiliya na kiSwahili cha kutengezwa, kiSanifu. Ṯafauṯi hii ni muhimu katika makala yetʰu kwa sababu inatupa uwezo wa kuzungumziya mambo ambayo yanakitʰa kwenye ṯafauṯi hii.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.803

**MWAND̪IKO KUT̪OKA WA KIARABU HAD̪I WA KILATINI**

Baad̪a ya kutambulika kwamba kusanifishwa kwa lahaja za kiSwahili ni lazima ili kuwapa wat̪awala wakoloni wepesi katika usimamizi wa makoloni ya Afrika Mashariki basi kukaunrwa Kamati ya Lugha iliyopend̪ekezwa katika mikutano ya 1925-1929 ili kusimamiya usanifishaji huwo (Whiteley, 1993). wanakamati walikuwa wazungu t̪u mwanzoni na baad̪aye sana wakashirikishwa wenyeji wa kiSwahili. Msingi wa usanifishaji iliamuliwa, kut̪okana na mapend̪eleo ya wat̪awala wakat̪i huwo – waArabu na wazungu, kuchukuwa lahaja ya kiUnguja mjini iliyokuwa imejaa kiArabu kingi na kuifanya nriyo lahaja it̪akayosanifishwa kwayo (Steere, 1919).

Kusanifisha lugha kulihit̪aji piya usanifishaji wa mwand̪iko wake au hati yake. KiAsiliya kina historiya nrefu ya kwand̪ikwa kwa hati ya kiArabu iliyofanyiwa marekebisho kukidhi saut̪i zake (Abdulaziz, 1979). Kulingana na Polome (1967) kwa sababu ya t̪aabu zilizojit̪okeza katika kutumiya hati ya kiArabu ambayo haikuwa na viwakilishi va saut̪i zot̪ʰe za kiasiliya basi waliyamuwa kugeuza kut̪oka hati ya kiArabu na kuanza kutumiya hati ya kiLatini. Msingi wa usanifishaji wa hati ya kiLatini ulichukuwa mwand̪iko aliwopendekeza Steere (1919) ambao piya ulijimili katika mat̪amshi yaliyokuwako Zanzibar mjini. Na palipokosekana kiwakilishi cha saut̪i basi alfabeti moja ilichukuwa pahali pa saut̪i kadhaa, kwa mfano, /t/ kuwakilisha saut̪i zot̪ʰe za [ t, tʰ, t̪, t̪ʰ ] au /d/ kwa [ d, d̪, ɗ, ɾ ].

Kazi ilofanywa na Kamati ya Lugha ni kubwa na ilijaribu kwa kad̪ri ya uweza wake. Mivutʰano katika mawanda ya kit̪aalimu mfano, Khalid (1977); mahojiyano aloyafanya Mazrui katika kupata data yake ya 'ukubalifu' wa kiSanifu miyongoni mwa waMvit̪a, na hat̪a Amour (2008) bado anaangaziya suala hili. Katika uchanganuzi wa khalid, Mazrui, Bakari, na wengineo walokuja baad̪a yao wameonesha umuhimu wa fonolojiya katika kwelezeya matatizo yat̪oka wapi katika ut̪amkaji na mwand̪iko wa kiSanifu. Nriyo hoja tunayoishikiliya sisi kuhusu kurekebisha mwand̪iko kut̪okana na uwamilifu wa saut̪i hizo kujit̪afaut̪isha na kut̪afaut̪isha maana ya maneno kulingana na matumizi katika kiAsiliya. Hata Mgullu (1999) ambaye ufunzaji wake ni wa kiSanifu bado ana sehemu katika kazi hiyo kuhusu kukiyand̪ika upya kiSanifu kut̪okana na kut̪owafikiyana na mat̪amshi.

**DHIMA YA FONOLOJIYA**

Kulingana na Lass (1984, uk. 23-4) fonolojiya ina jukumu la kweleza sifa bainifu za saut̪i za binadamu na kuzitambulisha. Zaid̪i, fonolojiya huweza kuonesha t̪afaut̪i ya maana inayopatikana kwa kulinganisha jozi za maneno. Sifa hii ya ulinganuwaji wa saut̪i na maana ni katika kuonrowa utata katika maneno na ikiwezekana kuonrowa uziyadadufu ambao haut̪afaut̪ishi maana. Bakari (1985:50) akimnukuu McIntosh (1961) anasema, "ufafanuzi kamili wa lahaja unahit̪aji maelezo kamili ya sifa zake zot̪ʰe amilifu za lahaja hiyo na namna kila kipashiyo kinavofanya kazi katika jumuiya yake'. Kwa mfano, /paka/ ni 'to color' lakini /pʰaka/ ni 'cat' . Vilevile, /fika, shika, lika, wika, rika, zika/ zinaonesha namna t̪afaut̪i ya saut̪i katika kila neno inaleta t̪afaut̪i ya maana – ina sifa ya kifonemiki. Lass (1984, uk. 22) anafafanuwa kuwa ikiwa kwand̪ika kifonolojiya kwahit̪ajika kuonesha tafsili ya fonimu yenye kuonesha ut̪afaut̪i fulani basi tafsili hiyo ijit̪okeze ili saut̪i hizo zitambulike kifonemiki.

Tufahamikiwe kuwa wasanifishaji walit̪aka kukifanya kiSanifu kiwe chasemeka, kwand̪ikika na kufahamika kwa wepesi kwa sababu ya matumizi yake mapana kwa ummah. Waliikataa hati ya kiArabu kwa sababu ya mbabaisho wake kujuwa ni neno lipi lizungumziwalo, kwa mfano, /g/ iliwakilishwa na /غ ق ك ج/ (Polome, 1967, uk. 200). Walifanya baadhi ya masuluhisho kutatuwa utata huwo wa /k, g, ng/ walakini waliweka uwamilifu wa saut̪i, kwa mfano, /t/ kanro na kuziwakilisha na alfabeti moja ya 't' /taa, tʰaa, t̪ʰawa, mti/ ambazo ni 'lamp, fishing basket, louse, tree' kwa mt̪awaliya huwo na utata ukabakiya palepale katika kukiyand̪ika kiAsiliya. Piya hawakwangaliya kima cha utumiyaji wa saut̪i hizo katika kiAsiliya; jambo walilolitiliya maanani wakat̪i wa kugeuza hati za kiArabu kwenra kiLatini. Fauka ya hayo, walipuuza t̪afsili za saut̪i na kuzifanya ni homofoni wakasahau kuwa zina uwamilifu wa kifonemiki. Bakari (1985) ameonesha umuhimu wa saut̪i katika utambulisho wa wasemaji wake na Mazrui (1981, uk. 130) alipata kwamba saut̪i hizi zina mafungamano na d̪ini ya wasemaji wake. Kwa mfano, neno /wadudu/ likit̪amkwa kiSanifu humaanisha 'insects' lakini

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.803

katika kiAsiliya /wad̪ud̪u/ humaanisha ‘jina moja la Mwenyezi Mungu’. Jedwali 1 linalofuwata lina mkusanyiko wa saut̪i, baad̪a ya uchanganuzi, zitumikazo katika kiAsiliya na mifano yake yanayoonesha uwamilifu wa kimaana.

**Jedwali 1: Fonimu za kiAsiliya na pend̪ekezo la mwand̪iko mpya**

| **Fonimu za KiAsiliya (Vitemwa)** | | |
|---|---|---|
| **Kiwakilishi** | | **Mfano Katika Maneno (herufi zenye mkolezo)** |
| **IPA** | **Pend̪ekezo la Mwand̪iko** | |
| [ a ] | a | /baba/ |
| [ e ] | e | /**e**l**e**za/ |
| [ i ] | i | /iliki/ |
| [ ɔ ] | o | /**o**g**o**pa/ |
| [ u ] | u | /**u**zi/ |
| [ p ] | p | /**p**aka/ (to color) |
| [ $p^{h}$ ] | $p^{h}$ | /**p**$^{h}$aka/ (cat(s)) /**p**$^{h}$a:/ paa (gazzelle(s)) |
| [ β ] | ʌ | /**β**era/, /**β**ara/ (ku-taka, ku-pata – Kivumba) |
| [ ð ] | dh | /**dh**ahabu/ |
| [ X ] | kh | /**kh**abari/ |
| [ ɣ ] | gh | /**gh**ali/ |
| [ θ ] | th | /**th**ala**th**ini/ |
| [ t ] | t | /m**t**i/ |
| **[** $t^{h}$ ] | $t^{h}$ | /**t**$^{h}$ava/ (stay indoors), /m**t**$^{h}$u/ (person), /**t**$^{h}$a:/ (fishing basket), /m**t**$^{h}$o**t**$^{h}$o/ (child), /n**t**$^{h}$a/ (wax), /ki**t**$^{h}$u/ (thing) |
| [ t̪ ] | ṭ | /**t̪**a:/ taa (light/lamp) |
| [ t̪$^{h}$ ] | ṭ$^{h}$ | /**t̪**$^{h}$ava/ (lice/louse), /n**t̪**$^{h}$a/ (point) |
| [ d ] | d | /**d**ada/, /pan**d**a/ (to climb) |
| [ d̪ ] | ḍ | /**d̪**ara/ (touch), /fun**d̪**i/ (craftsman), /pan**d̪**a nguwo/ (to fold up the robe), |
| [ f ] | f | /**f**uwa/ |
| [ h ] | h | /**h**aribu/ |
| [ ħ ] | h | /**h**ali/ |
| [ v ] | v | /**v**uta/ |
| [ ʧ ] | ch | /**ch**ama/, /**ch**oo/ (toilet) |
| [ $tʃ^{h}$ ] | $ch^{h}$ | /**ch**$^{h}$ungu/ (black ant), /**ch**$^{h}$oo/ (worm) |
| [ k ] | k | /kaka/ |
| [ $k^{h}$ ] | $k^{h}$ | /**k**$^{h}$a:/ (crab) |
| [ s ] | s | /sasa/ |
| [ z ] | z | /**z**umari/ |
| [ l ] | l | /lala/ |
| [ ʒ ] | ʒ | /buʒu/ (fool), /nʒumaa/ (type of tea leaf) |
| [ ʃ ] | sh | /**sh**ati/ |
| [ r ] | r | /**r**uka/ |
| [ m ] | m | /mama/ |
| [ n ] | n | /**n**u**n**uwa/ |
| [ n̪ ] | ṇ | /**p**an̪a/ (panya ‘rat’), /**n̪**ama/ (nyama ‘meat’) |
| [ ɱ ] | m | /mvuwa/ |
| [ ɲ ] | ny | /nyanya/ |
| [ ŋ ] | ng’ | /**ng'**ombe/, /ankuja/, /anketi/ |

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

| **Fonimu za KiAsiliya (Vitemwa)** | | |
|---|---|---|
| **Kiwakilishi** | | **Mfano Katika Maneno (herufi zenye mkolezo)** |
| **IPA** | **Pend̪ekezo la Mwand̪iko** | |
| [ j ] | y | /yaya/ |
| [ w ] | w | /**w**asili/, /sugu**w**a/ |
| [ w̪ ] | w | /**v**e**v**e/ (you), /**v**atu/ (people), /**v**ali/ (rice) |
| [ ŋg ] | ng | /**ng**amiya/ |
| [ mb ] | mb | /**mb**ali/ (far) |
| [ ŋz ] | nz | /**nz**uri/, /**nz**ima/ |
| [ ŋʥ ] | nj | /n**j**ema/, /n**j**iya/, /n**j**o:/ |
| [ ŋɾ ] | nr | /**nr**izi/, /**nr**ani/, /**nr**o:/ (pail) |
| [ n̪d̪ ] | ṇḍ | /**n̪d̪**iya/, /**n̪d̪**a:/, /**n̪d̪**aki/, /**n̪d̪**o:/, /**n̪d̪**ovu/ |
| [ t$^r$ ] | t | /t$^r$ango/, /t$^r$wanga/, /chapat$^r$i/ |
| Vibwakiya | | |
| [ ɓ ] | b | /**b**a**b**a/, /**b**i**b**o/, **b**i**b**i |
| [ ɓ̇] | ɓ̇ | /**bw**ana/, /**bw**i**bw**i/ (dumb person) |
| [ ʄ̇ ] | ʄ̇ | /**j**ana/, /**j**ambo/ |
| [ ɠ ] | g | /**g**ari/, /**g**engi/, /**g**uu/, /**g**oti/ |
| [ ɗ ] | ḍ | /**d̪**alili/, /**d̪**angana/, /**d̪**ari/ |
| [ ƥ ] | ṗ | /**pw**a:/, /**pw**elewa/, /**pw**eke:/ |
| [ ƙ͡ƥ ] | k̇ | /ya**kwe**/, /wa**kwe**lako/, /m**kwe**/, /m**kwa**ju/ |
| [ ɠ͡ɓ ] | ġ | /chun**gw**a/, /pi**gw**a/, /fun**gw**a/ |
| [ ṁ] | ṁ | /**mw**alimu/, /**mw**ana/, /ka**mw**e/, /zi**mw**i/ |

Jedwali hili limeorodhesha saut̪i tulizochanganuwa kut̪oka kwa Bakari (1985), Polome (1967), Mazrui (1981), Hayward na we. (1989) Nurse na Hinnebusch (1993), na Lodhi (h.t) na utambuzi wet$^h$u wa kit̪ajriba. Piya kwa kumfuwata Lass (1984), tumeengeza t̪afsili katika fonimu hizo ili zioneshe uwamilifu wa kifonemiki. Tumejaribu kut̪owa piya pend̪ekezo la mwand̪iko katika othografiya mpya ya kiSanifu. Saut̪i za kaakaa laini md̪omoni zit̪awakilishwa na [ ˙ ] na kit$^h$one cha juu kwa mfano [ṁ]. Saut̪i za menoni kit$^h$one hicho kit̪awekwa chini [ḍ , ṭ]. Saut̪i ambazo zina sifa ya mpishano huru, yaani hazileti t̪afaut̪i ya maana, kama [ħ], [w̪], [ʒ], na [ɓ, ɗ, ɠ ] zit̪atumiya saut̪i zilezile zinazotumika kwa sasa [h, w, z, b, d, g]. Saut̪i [β] yapatikana katika chiChifund̪i na kiVumba t̪u yaweza kuwakilishwa na [ ʌ ]. Popot$^h$e pale penye uwamilifu wa kubad̪ili maana tumet̪afsiri kwa kiIngereza ili t̪afaut̪i hiyo iyonekane ikilinganishwa na kiSanifu, kwa mfano, [t̪$^h$awa] (louse) na [t$^h$awa] (stay indoors). Katika jedwali hili hatukushughulikiya irabu nrefu ijapokuwa zina uwamilifu wa kubad̪ilisha maana, kwa mfano, /d̪ua/ (prayer) na /d̪uwaa/ (astounded). Tuliyepuka matumizi ya ritifaa [’] katika mwand̪iko kwa sababu ya okosowaji wa Mbaabu (1985) kuhusu alama hiyo ijapokuwa Abdulaziz (1979) aliitumiya kut̪afaut̪isha mpumuwo katika mashairi ya Muyaka. Nilitumiya ukurasa wa IPA katika wikipedia.org kupata uhakika wa saut̪i hizi na piya utambuzi wet$^h$u.

## Mafungamano ya Fonolojiya na Hati

Katz na Frost (1992) ameeleza namna fonolojiya inavoingiliyana na hati na amekuja kuonesha namna neno linavoand̪ikwa kihati huweza kuathiri utambuzi wa neno kwa msemaji wa lugha hiyo. Utambuzi huu unat̪okana na fonolojiya iliyomo bongoni mwa msomaji na mnenaji. Wanafunzi wachanga au hat̪a wat$^h$u wazima wanapoliyona neno namna lilivoand̪ikwa hutambuwa ni fonolojiya ya lugha yake ama ni fonolojiya ngeni kama ‘alivomaka’ Bakari (1985, uk. 85) alipochanganuwa data ya chiChifund̪i na kiVumba kuhusu kuingizwa konsonanti /w/ katika kauli ya kutenrwa (rejeleya ufafanuzi wet$^h$u wa saut̪i ya kaakaa laini md̪omoni kuhusu fonimu hii).

Kina kikiwa cha maonroni, yaani, saut̪i za lugha hiyo na alfabeti yake kuna mnasaba wa moja kwa moja – inavot̪amkwa nrivo inavoand̪ikwa – basi

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.803

utambuzi wake uṯakuwa rahisi. Katika kiSwahili /i/ ni /i/ kokoṯʰe uṯakakoikuta: mwanzo /ita/, kati /aṯika/ au mwisho /kati/. Akaṯafautisha na lugha ambayo mwanḏiko wake ni wa kina kirefu ambapo – kiṯamkwavo sivo kiyanḏikwavo. Kwa mfano, tukichukuliya wasomeshwavo wanafunzi wa msingi maskulini huku Kenya, tuṯaona wakiyambiwa ‘c for cat’ (pʰaka). Lakini ‘c’ hiihii ikija mara nyingine hugeuka na kuṯamkwa /s/ kwa mfano, /elektrisiti/ ‘kaharabai’ au /siti/ ‘mji mkuu’ japo huanḏikwa ‘electricity’ na ‘city’. Mfano wa kiirabu ni watoto wa madarasa ya chini wanapofunzwa sauṯi za kiIngereza huambiwa ‘i for insect’. Halafu mtoto wa kiSwahili anapokutana na sauṯi hii katika ‘ice-cream’ /aiskrim/ aweza kulisoma neno hili /iskrim/; kwa sababu katika kiSwahili /i/ huṯamkwa hivohivo wakaṯi woṯʰe. Kwa hivo, kwa sababu ya mithali ṯu, kiIngereza ni yenye hati ya kina kirefu kwa kuwa kiyanḏikwavo sivo kisomwavo (Katz na Frost, 1992). Nriposana Polome (1967, uk. 208), alipokuwa akizungumziya ujifunzaji wa vokali za kiIngereza, akasema kuwa mwanafunzi wa kiSwahili akijifunza kiIngereza hujumlisha irabu zoṯʰe 15 za kiIngereza na kuziṯamka kama zile 5 za kiSwahili.

### Huṯamkwa yoṯe yonṯe au yoṯʰe?

Bakari (1985, uk. 161) anasema kwamba hajapatapo kuwona uṯafiṯi unaozungumziya kupatikana katika sauṯi moja, mpumuwo na umenoni. Yaani, sauṯi /ṯʰ/ ya /ṯʰawa/ ‘louse/lice’. Kunao waliyojiṯokeza kwelezeya kwamba huku kumenonisha kumeṯokana na lugha za kiKushiti ambazo ni jirani sana ya lugha za lahaja za kaskazini ya Kenya: kiAmu, kiṮʰikuu, kiSiyu (Nurse, 1985) ama ni mkopo kutoka kiArabu kulingana na Bakari. Kwa hivo, lahaja hizo ziliathirika na kiKushiti na kutʰangaa kusini kufikiya Mviṯa.

Nadhariya tʰetʰe nyengine ni kwamba kumenonisha huku kuliṯokeya kusini kwanza katika nchi za Tanzania, Democratic Republic of Congo na maeneo hayo ya maziwa makuu halafu ikatʰangaa kaskazini kufikiya kiSwahili (Janson, 2007). Na wanaonesha kwamba sauṯi hizi zilibadilika kuṯoka kuwa vizuwiyo-vikwamizo na kuwa za ufizini, kwa mfano sauṯi /ts/ katika /tsalafu/, /tsana/ na kwa kiAsiliya kuwa /siyafu/, /ṯana/, ‘black ant’ na ‘to comb’ kimṯawaliya. Tuṯaona hapa kwamba /ch/ iligeuka na kuwa /t/ baadaye kuwa /ts/ lakini kwa kiAsiliya ilisonga mbele na kuwa ya /ṯ/ ya menoni. Au wengine wasema labda iliṯoka /ch/ na kuruka kuwa /ts/ mara moja. Kwa kiAsiliya ni alivosema Nurse (1985, uk. 245) kuwa mfanyiko wa kuivuta mbele zaidi sauti /ts/ ulifanyika na ikawa /ṯ/.

Tukija kwenye mfanyiko wa kimofofonolojiya wa kupumuza (kuweka mpumuwo pahala pasipo mpumuwo) tuṯaona kuwa Bakari (1985, uk. 66 & 253) anasema kwamba asili ya kupatikana mpumuwo, kwa mfano, katika ngeli ya N – N katika nomino /kamba/ ikawa /kʰamba/ ni kwamba inafahamika kuwa asili ya neno lenyewe lilikuwa na /N+kamba/ lakini muḏa ulipopita iligeuka na kuwa /kʰamba/. Kwa hivo mpumuwo huwo umeṯokana na kusimilishwa hiyo /N/ na kuwa mpumuwo. Walakini haya ni maelezo ya mpumuwo unaopatikana katika mwanzo wa nomino lakini hajapata maelezo ya mpumuwo huu kuja katikati ya neno au mwishoni.

Ufafanuzi wetu juu hilo unaṯokana na uṯendi maarufu wa *Hamziyah*. Mfasiri anasema hivi:

> *1. Hali wakwelaye kukwelako mitume* ***yonte***
>
> *Uwingu usiwo kulotewa ni moya sama?*
>
> *88.**Wonte** wo watano wasibiwa kwa ndwele kuu*
>
> *Na kuhilikika auniye ni ndwele jama.*

Katika beti hizi mbili tulizonukuu kuṯoka wa Mutiso (2005, uk. 111 & 161) na Olali (2008, uk. 43) tuṯaona pametumika maneno mawili /yonṯe/ na /wonṯe/. Katika fasiri yake wa Mutiso uk.40 anatweleza kuwa ni lahaja ya Chimiini ambayo hutumiya maneno hayo na kwa kiSanifu maneno hayo ni /yote/ na /wote/. Lakini ukiwasikiza waSwahili asiliya wanayaṯamka /yotʰe/ na /wotʰe/. Yaani kuna mpumuwo umeingiya kati na hiyo yaelezeka kwa kuonroka /n/ na kufanywa sauṯi ya kupumuza /tʰ/ mbali ya kwamba ni sauti ya menoni piya. Mfanyiko huu ni ule ule ulosababisha mpumuwo katika nomino za N – N.

### Je, sauṯi ya kaakaa laini mḏomoni ipo katika kiAsiliya?

Kulingana na CASAS (2012, uk. 7) sauṯi hii ya kaakaa laini mḏomoni haipo katika kiSanifu. Katika jedwali walilochora yaonesha sauṯi hii iko katika

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.803

kiMijikenra ṯu. Nurse na Hinnebusch (1993) wanasema kwamba sauṯi hii /kp/, /bp/, /ŋm/ ipo katika kiSanifu na kiAsiliya na huwakilishwa kihati kama sauṯi mwambatano /kw/, /bw/, na /mw/. Katika uwainishaji wa CASAS unaonesha sauṯi /mw/ ni ya miḏomoni. Walakini katika uṯafiṯi ulofanywa na Clements na Sylvester (2002) kuhusu sauṯi hii ya kaakaa laini mḏomoni wamekuja kuonesha kwamba sifa zoṯʰe bainifu za kuṯamkwa kuwili kwa mara moja, upasuwo, ubwakiyaji, presha ya pumzi nrani ya mḏomo, na kushuka na kupanra kwa koromeo si lazima ziweko katika kuṯamka sauṯi hizo. Fauka ya hayo, Nurse na Hinnebusch (1993, uk. 174) wanasema kwamba sauṯi hizi zaṯamkwa viyungani mwa Mambasa, kwa mfano, Jomvu. Mimi nimezisikiya sauṯi hizi kwetu Mji wa Kale (sehemu ya Lango la Pʰapa hadi Allidina School, Mambasa) kuliko na kiAsiliya na zina sifa ya kubwakiya pʰumzi baḏala ya kupasukiya nje. Twelewe kuwa sauṯi hizi zimedhihirika kuṯokana na mifanyiko ya kimofofonolojiya, kiini cha uṯafiṯi wa Bakari (1985), na yaonekana wasanifishaji walizitambuwa sauti hizi, na kwa kuziwakilisha kialfabeti wakazifanya sauṯi mwambatano kwa mfano, /kw bw pw mw/. Bakari (1985, uk. 84) akimnukuu Hyman anayemnukuu Jakobson (1941) anasema kwamba mpangiliyo wa silabi wa lugha za ulimwenguni ni KVKV. Bakari (ukurasa 75) anasema usahilishaji nriyo hali asiliya wa lugha na katika kiAsiliya wanenaji wake husema /dhombo dhangu/ kiṮʰikuu, /zombo zangu/ kiAmu na /vombo vangu/ kiMviṯa baḏala ya /vyombo vyangu/ kiSanifu yenye /vy/ kinyume na asemavo Bakari (1985, uk. 183) kwamba kiAsiliya ni usahilishaji wa kiujana. Uṯafiṯi wetʰu unaoneleya utambuzi wa sauṯi hizi za kaakaa laini mḏomoni zilijulikana na waanḏishi wa kiSanifu na wakashinrwa kuzipa viwakilishi va alama moja ya alfabeti ikabiḏi wazitiliye /w/ kufuwata kiIngereza ambayo kwake ni sauṯi ya kaakaa laini. Ushahiḏi mwengine wa hakuna /w/ katika neno /pʰwani/ yenye dhana ya ‘maji’ katika kiAmu na ambayo katika lugha za kibara ya Kenya huitʰwa /peek/ kiKalenjin, /pii/ kiJaluo, /biyo/ kiKushiti (mazungumzo na Dkt. A. Roṯich, idarani, UoK). Tuṯaona katika lugha hizo za kibara, ambazo nrizo kiyelelezo cha lugha za kiAfrika, kufuwata hoja ya Chambers na Trudgill (2004, uk. 41) ya kupima ufanano wa lahaja, kuna /p/ na /b/ (ghuna ya /p/) na hazina /w/, hivo, kutwangaziya sababu nyengine ya kukataa othografiya ya kiSanifu yenye kukutanisha KK katika neno. Nriposana, Mwita (2007) ameitaka IPA izitambuwe sauti mwambatano za kiSanifu /nz/, /mb/, /nj/, /nr/, zinazopatikana piya katika kiAsiliya, kuwa sauṯi moja nasi twapenḏekeza hali kadhalika kutambuliwa kwa sauṯi hizi za kaakaa laini mḏomoni na kwanḏikwa upya katika kiSanifu kama tulivofanya katika Jedwali 1.

Kwa minṯarafu hiyo basi, ikiwa othografiya ni uwasilishi wa lugha ya kunenwa kwa maanḏishi (Milroy & Milroy, 1999) na kwamba sauṯi za kiSwahili zina uwamilifu wa kuṯafauṯisha maana kifonolojiya, hazina buḏi basi kujumuishwa katika alfabeti yake ili wanafunzi wa lugha hii wasibabaishwe na kuona neno laanḏikwa vengine na laṯamkika vengine. Kwa mfano, Kamusi la Kiswahili Fasaha (2010) walijaribu kuungamanisha sauṯi katika kuanḏika vidahizo vao lakini hawakuzijumuisha katika hati ya vidahizo hivo. BAKIZA wamesema kuwa wamefanya hivo kuhifadhi uwasili wa kiSwahili chao, lakini, kama Mazrui (1981) alivopata ufungamanisho wa sauṯi na dini, na Barwani (1995) aliyanḏika ṯafsiri yake ya *Kuruwani* (kitabu kitʰakatʰifu cha waIslamu) ya *al muntakhab* namna alivoṯamka maneno hayo.

## Fonolojiya na umiliki wa lugha ya pili

Musau (1994) katika uṯafiṯi wake kuhusu ujifunzaji lugha ya pili na walimu wa masomo hayo amekuja kuonesha umuhimu wa fonolojiya katika kadhiya hii. Baadhi ya umuhimu alisema ni: usomaji wa uṯamkaji ni muhimu katika kweleweka na unaowasiliyana nao; uṯamkaji muwafaka una umuhimu wa kijamii kwa sababu ya kuepuka miyelekeo hasi baina ya wanajamii; na usomaji wa sauṯi uṯamsaidiya mwalimu kutambuwa hiṯilafu na kuṯowa mbinu za kurekebisha hiṯilafi hizo katika darasa la lugha. Kimaoni ya Musau njiya ya kuzifahamu sauṯi kwa uwasilishaji wa juu nriyo muwafaka katika ufunzaji lugha ya pili kwa sababu ya uwazi wake wa sauṯi hizo kujulikana. Anaoneleya si sawa kutumiya njiya ya uwasilishaji wa chini kwa sababu mbinu hii huepuka sifa bainifu kadhaa za sauṯi na hivo kuṯompa mwanafunzi ufaṯashi mzuri wa makosa ya uṯamkaji wa lugha lengwa. Piya, anasema sauṯi isiposikika au kwandikika vizuri basi sauṯi hiyo iṯajulikana kibahaṯi nasibu.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

East African Journal of Swahili Studies, Volume 5, Issue 1, 2022
Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.803

***CBC na jamii-ṯengwa***

Tukichʰangiya zaiḏi hoja ya fonolojiya katika elimu, hivi sasa nchini Kenya kuna mṯalaa mpya wa elimu unaoitwa Mṯalaa wa Umilisi (Competence Based Curriculum [CBC]) unaoṯekelezwa na Kenya Institute of Curriculum Development (KICD) katika ṯaalimu yoṯʰe – kwanziya msingi, upili, na chuwo kikuu – ambao unatiliya nguvu usomeshaji wa lugha za kwanza katika miyaka mitʰatʰu ya kwanza ya shule za msingi. Sehemu ambazo zina wasemaji wengi wa lugha fulani wanafunzi hao hufunzwa kwa lugha hiyo na sehemu ambazo ni wingi-jamii basi kiSwahili kiṯafunzwa hapo. Mose (2017), wa Mberia (2016) woṯʰe wameonesha kwamba uṯekelezaji huwo bado haujafaulu kwa sababu ya miyelekeo, mipangiliyo ya kiuṯekelezi, lakini msimamo wetʰu ni kwamba na walimu wenyewe bado hawajaṯayarishwa vizuri kuhusu lugha wanazokwenra kukumbana nazo nyanjani.

Katika maeneo ya Pwani kusemwako kiAsiliya walimu huwa baadhi ni wa kuṯoka sehemu hizo lakini piya kuna wengi ambao si wa sehemu hizo. Pili, walimu hawa waliṯayarishwa kufunza kiSanifu na wanafunzi wanaokwenra kukutana nao ni wanafunzi ambao nriyo sasa wameṯoka majumbani mwao wamekuja shule, hivo, bado wana lugha zao za kiAsiliya. Na katika makala haya tumeonesha namna sauṯi nyingi zenye umuhimu wa kifonolojiya hazimo katika kiSanifu. Wanafunzi hawa lazima waṯatatizika wanapofunzwa vengine na wao wanajuwa vengine kuhusu sauṯi hizo. Kwa mfano, mtʰotʰo wa miyaka mine aambiwe ‘usiseme /ṯaa/ ‘lamp’ hivo ni makosa, sema /tʰaa/’ (Munyaya, 2019). Ambapo yule mtʰotʰo anajuwa kwamba /tʰaa/ ni mkoba wa kuchukuliya vitʰu kule nyumbani kwao. Kwa hivo, mazingira (lugha) ya nyumbani yaliyokusudiwa ayapate shuleni hayapati na hivo kumtiya mtʰotʰo katika wahaka wa kiuṯamaduni (wa Mberia, 2016).

La zaiḏi, ni kwamba nyenzo za ufunzaji za lahaja hizi hazipo kwa sababu KICD, labḏa haijaona umuhimu wa kushughulika na lugha hizi za jamii ya watu hawa kama vile wafanyavo kuhusu lugha za jamii nyenginezo. Kwa mfano, hutangaza haswa kuanḏikisha waanḏishi wa lugha ‘asiliya’ zilizoṯeuliwa na wao za kufunzwa katika kiwango hicho na kiAsiliya hakimo katika orodha hiyo (Gekonge, 2021). Au, kama tulivokwisha kusema hapo awali, labḏa KICD imechukuliya kuwa kiAsiliya piya ni kiSanifu na kuzibanrika jina moja: zoṯʰe ni kiSwahili. Uṯafiṯi wetʰu umechanganuwa kuwa, kwa kuṯojuwa mambo yangegeukaje Kenya, Mbaabu (1985) alipinga haya ya kusanifisha ṯena kiSanifu kwa sababu hakina ṯafauṯi za kiisimu haṯa akaghafilika kusema kwamba sauṯi hizo hazileti ṯafauṯi yoyoṯʰe ya kimaana (ukurasa 175); na pili, alikataa kwanḏikwa lahaja sanifu upya kwa sababu ya gharama kubwa ya kifedha inayohiṯajika kuwaita waanḏishi waanḏike lahaja hiyo (ukurasa 207). Twadhani, wakaṯi wa kwanḏika kwake Mbaabu lilikuwa wazo hilo baḏo halijafikiriwa na KIE (sasa KICD) kuhusu kuzianḏika lugha za kiasiliya za Kenya. Miyongo mitʰatʰu baaḏaye, kwa kufuwata Kaṯiba Mpya ya 2010 lugha za kiasiliya zimetambulika na wazo la kuzifunza katika madarasa ya chini limepokelewa na kuṯekelezwa na Wizara ya Elimu.

Tufahamu, ikiwa ni uwasiliya, basi Chimerah (2020), baaḏa ya fikira kujiṯokeza katika kongamano la kujaḏili Mswaḏa wa Lugha za Kenya 2015, amesema kuwa lazima lahaja hizi za kiAsiliya za Pwani zipawe hadhi kama lahaja nyenginezo, kwa mfano za kiMijikenra, kuwa ni ‘lugha za kijamii’ kwa sababu hazifanani kiuṯamaduni, kihistoriya na kimaṯamshi na kiSanifu. Na haya ya kutambulika na kushirikishwa lahaja/lugha za hadhi ya chini kwa sababu ya ubaguzi wa rangi, ṯabaka, kabila yanaenrelezwa na iṯikadi ya lugha ambayo Milroy na Milroy (1999) wanasema si sababu za kiisimu bali ni sababu ya kiṯaasubi ya usanifishaji. Wanasema kuwa lugha ya waAfrika wa kiAmerika ilichukuwa muḏa mpaka ilipokubaliwa kwenye mfumo wa elimu katika majimbo fulani, likiwamo la Oakland, California. Ubaguzi wa aina yoyoṯʰe hausṯahili katika elimu kwa sababu ‘ujumuishi’ katika elimu, kulingana na UNESCO (h.t), ni kuepuka aina ya ubaguzi wowoṯʰe wa kiṯabaka, kikabila, kirangi, kiḏini, na haṯa kiuwezo wa kimaṯamshi. Hivo, KICD wana jukumu kuṯimiza malengo ya ulimwengu sawiya ya nchi ambayo inakwenra mbiyo kwepuka kufurika ‘lava ya ubaguzi’ katika wingi wetʰu (Mutambo, 2021).

## KIASILIYA KATIKA ZAMA ZA NUKṮA

Kwangaziya suala hili tuṯalijibu kiwili: kiAsiliya kiṯafaiḏishaje kiSanifu kwa kutumiya teknolojiya; na pili, kiAsiliya kiṯajifaiḏishaje kutumiya

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.803

teknolojiya kujiokowa. Mfumuko wa teknolojiya ya habari na mawasiliyano (TEKNOHAMA) katika zama hizi zimeleta mabad̪iliko makubwa katika sekta zot̪ʰe za maisha ya mwanadamu, na ya elimu haikusazwa. Juu ya hayo, kuingiya kwa tanravu la COVID 19 mwelekeo wa kielimu hivi sasa umefanya ut̪egemezi wa teknolojiya ni mkuu mno. Mifumo ya uwasilishaji wa mad̪arasa imebad̪ilika na matumizi ya wingi-jihazi kufikisha ujumbe wa mwalimu nriyo uloshamiri sasa.

Teknolojiya imekuja ili kutusahilishiya ufanyaji kazi katika maisha yetʰu. Katika zama hizi za nukt̪a kila kʰitʰu kimepawa hesabu fulani katika t̪arakilishi had̪i majuzi kikohozi cha Korona kilitambulika siyo kwa shikiyo la dakt̪ari bali kut̪okana na algoridhimu ilopawa kikohozi hicho (BBC, 2020) kwa upekee wake. Tukumbuke hati za IPA piya zina t̪arakimu zake mahsusi – kila saut̪i ina namba yake ya kuitambulisha. Kut̪okana na hayo, kiAsiliya kinaweza kuchanganuliwa na kuwekwa kwenye ala za kit̪arakilishi ili kifaye wanaot̪aka kuzisikiya saut̪i hizi kwa ufasaha wa kimitambo. It̪asaidiya walimu na wanafunzi hali kadhalika ummah wot̪ʰe ut̪akaot̪aka kuzijuwa saut̪i, mat̪amshi yake, na kwaweza kutengezwa hat̪a kanra za video na saut̪i ili kuwapa mukt̪adha kamili wa matumizi wa mat̪amshi hayo au mitʰongoo yake. Kenya imebarikiwa na makunri ya lugha mane: kiBantu, kiHamiti, kiHamiti-mluwo, kiKushiti na lugha hizi zinazo saut̪i tunazozipend̪ekeza zifunzwe katika mashule ya Kenya hivo, hait̪okuwa t̪aabu kubwa sana kwa wanafunzi kutambuwa saut̪i hizi na kuzitiya katika uwamilifu unaofaa kinyume na alivohofiya Mbaabu (1985). Tukumbuke piya, t̪afsiri siku hizi ni za mashine zenye kulenga saut̪i na maand̪ishi hivo mitambo ya mitanrao inaenreleya kujit̪imiliza kuzijuwa saut̪i za lugha maarufu duniyani na kurahisisha kuzipata saut̪i za lugha hizo kwa wepesi. T̪arakilishi ikiweza kunakili saut̪i sawasawa (katika ut̪afit̪i ulofanywa 95% ya uhakika ilipatikana [Bigi na we., 2012]) basi na t̪afsiri mashine ya lahaja zot̪ʰe za kiSwahili zit̪aweza kut̪afsiriwa kwa ufasaha kinyume ilivofanyika zama za mashine ambazo 'hazijafunzwa' lugha hizo.

Kwa mnasaba huu wa TEKNOHAMA, kiAsiliya kinawezaje kujiokowa katika hali ya sakarat̪il maut̪i iliyomo hivi sasa? Crystal (2003) amepend̪ekeza kwamba kuziokowa lugha au hat̪a lahaja (kwake yeye anaona pana uwa t̪epet̪evu unaogawa dhana hizi mbili) zinazozungumzwa na watʰu wowot̪ʰe ulimwenguni pana haja ya ukereket̪wa na uwanaharakat̪i wa wasemaji wake ili kukihifadhi. Mwanzo kutambulika halafu kujit̪okeza redioni, magazet̪ini na kʰumbi mbalimbali, na kukitiya katika mfumo wa elimu ni kati ya mbinu zinazoweza kukifanya kibakiye katika sura ya ulimwengu. Lakini, juu ya mbinu zot̪ʰe hizo, hakuwacha kutaja matumizi kikamilifu ya teknolojiya katika kuhifadhi nyaraka, kukiand̪ika, na zaidi kutumiya video na vinasa saut̪i na kukiweka katika mitanrao mahasusi ya lugha hizo iliyobuniwa kwa ajili ya lugha hizo. Piya, kuhimiza kizazi kichanga kijivuniye lugha yake na kukitumiya kila wakat̪i kila mahali. Juhud̪i za kipwekeepwekee za mashirika yasiyo ya kiserikali katika kukihifadhi kiAsiliya ni akali ya mambo lakini bad̪o pana kazi kubwa haswa kut̪oka kwa serikali ambayo ina rasilimali nyingi za kuwekeza katika kukihifadhi. T̪angu alipoand̪ika Mbaabu mwaka wa 1985 amelikazaniya hili la kuwa na mfano wa BAKITA, BAKIZA (chembelecho Chimerah (2020) BATAKIKE liwe la Kenya) ambalo lit̪achukuwa usukani wa kuyaenresha mambo ya lugha hii nchini. Ni miyaka zaid̪i ya mitʰatʰu sasa t̪angu likubaliwe na serikali ya Kenya kuunrwa lakini mpaka leo baraza halijazawa.

## UWOKOZI WA KIASILIYA NA KISANIFU

Katika kazi ya Massamba na we. (2004) na Lodhi (2003) wameonesha namna kigezo cha mpumuwo kilivo na uwamilifu katika lahaja ya kiAsiliya na kiSanifu katika eneo la ut̪afit̪i wao, Tanzania. Hat̪a imepelekeya Massamba na we. kworodhesha saut̪i zenye mpumuwo katika jedwali la kiSanifu, jambo ambalo Musau (1994) amesema halijit̪okezi. Kazi ya Bakari (1985) ya lahaja za Kenya wakat̪i wa uchanganuzi wa data yake ameonesha uwamilifu wa mpumuwo lakini 'alipochora ramani za konsonanti' (na zimerejelewa ramani hizo na wat̪afit̪i waSwahili asiliya Timammy (2002) na Swaleh (2017)) hakuziweka kwenye majedwali yake kinyume na mtangulizi wake Abdulaziz (1979, uk. 76) ambaye aliziorodhesha saut̪i hizo katika jedwali lake. Yaonekana sababu zilizokuwa zikit̪olewa kuhusu kut̪oziingiza saut̪i za mpumuwo katika mfumo wa kiSanifu, ni kwamba "wasemaji wengi wa Bara pengine wanapata tabu kuvitofautisha vitamkwa hivyo ingawa wako baadhi wanaoweza, lakini je, hiyo ni sababu ya kutosha kuviondowa vitamkwa

hivyo kwenye orodha ya vitamkwa sanifu vya lugha ya kiSwahili?" Massamba na we. (2004, uk. 42). Suala la wengine kuṯoweza kuziṯamka sauṯi fulani au wingi wa wasiyoweza au wasiyoṯaka kuzitamka sauṯi hizi pambanuzi (Mbaabu, 1985, uk. 178), kulingana na Massamba na we., si sababu ṯoshelezi ya kuziwacha kuziweka katika kiSanifu.

Tukiyengezeya kuhusu ufungamanisho wa fonolojiya na othografiya, Bakari (1985, uk. 262) analalama kuhusu wanaoanḏika maneno ya kiSanifu na kufuwatanisha irabu mbili kwa pamoja, au, kama mṯafiṯi huyu alivoona kwengine irabu t$^h$at$^h$u (mfano, /kuiona/, /kuiangaliya/) jambo ambalo kifonolojiya ya kiSanifu haikubaliki na haṯa kimaṯamshi ya kimaumbile ya lugha hii haikubaliki. Anasema Lass (1984, uk. 98) uzuri wa uṯamkaji ni uchache wa kuṯamka na Bakari (1985, uk. 262) akaengeza ni ule unaopunguza ufuwatanisho wa sauṯi zaiḏi ya mbili za jamii moja (mfano irabu mbili) kwa pamoja akimfuwata Martinet na 'kanuni ya uchache wa juhudi' au uchumi katika kuṯamka. Umbile la kiSwahili ni la kiBantu linalokubali mfumo wa KVKV katika maneno yake; inapotokeya kuwako KKV basi kiSwahili hupachika vokali ili iregee kwenye asili yake ya kiBantu. Kwa mfano neno /shukran/ huṯamkwa /shukurani/. Ufuwatanisho wa KK (/-kr-/) umevunjwa na kufanywa KVKV (/-kura-/). Vilevile, mfanyiko wa kimofofonolojiya wa kuweka kiyayusho katika mwisho wa neno ni jambo aliloliyangaziya Bakari na lapatikana katika kiAsiliya choṯ$^h$e kwanziya Vanga haḏi Kiunga katika Mkowa wa Pwani ya Kenya. waSwahili hawo husema /ingiya/ na /pumuwa/ ambayo yaambatana na kinavoṯamkika (Polome, 1967, uk. 15 & 48) hivo kukubali lalamiko la Bakari kuhusu uwanḏishi wa lugha kinyume na maumbile ya uṯamkaji wake.

Tumeona kwamba baada ya uṯafiṯi mpana wa wazawa wa kiAsiliya katika upwa wa nchi ya Tanzania, waṯaalamu wa huko wameoneleya haja ya kugeuza jedwali la fonimu za kiSanifu Massamba na we. (2004, uk. 41). Bakari (1985) anasema kuwa sifa bainifu k$^h$uu ya lahaja zoṯ$^h$e za Kenya ni umenoni – sauṯi zinazoṯamkwa nyuma ya meno ya juu. Waṯaalamu wenzet$^h$u wa Tanzania wamechunguza na kukut$^h$a mpumuwo kwao nriyo *imeshamiri sana* (msisitizo wangu) (kinyume na alivosema Polome [1967, uk. 39] kuwa imeanza kupoṯeya) kefu huku Kenya ambako ni mpumuwo, na umenoni? Je, huu si mchanga mmoto kwa waṯaalamu wa Kenya kwangaliya upya uwanḏishi wa kiSanifu na kuziṯangamanisha katika hati yake ili iweze kuit$^h$wa ni iṯikadi ya lugha ya Kenya kama ilivo katika kiIngereza: kuna cha Amerika na cha Wingereza? Au, kama wafanyavo waYoruba kuṯaka kukiyanḏika upya kiYoruba (British Library, 2020) ambacho kimo haṯarini kama kiAsiliya. Lugha ya ṯaifa ni kama benḏera ya ṯaifa, asemavo Chris Wanjala akinukuliwa na Mbaabu (1985, uk. 187) na kila nchi ina yake japo wamo nrani ya jumuiya ya Afrika, Madola, Ulaya. BAKIZA wameliita kamusi lao Kamusi la Kiswahili Fasaha (2010), TATAKI wameliita kamusi lao Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2013) seuze Kenya nayo ikichukuwa barabara yake kuikuza lugha yake rasmi na ya ṯaifa ya kiSwahili yenye miyonroko yake huku ikipiganiya kujisawazisha na kiSwahili choṯ$^h$e cha mashariki ya Afrika.

## HIṮIMISHO

Kwa kutumiya TEKNOHAMA katika kukiyandika upya kiSanifu ikichangamanisha na uṯamkaji unaoch$^h$angiwa na kiAsiliya tumeonesha kuwa kiSwahili kwa jumla kiṯafaiḏika kuileta lugha karibu na unenaji wake na kuonrowa utatanishi wa kimaana hivi sasa kwa sababu ya uṯamkaji huwo. Naṯija iṯapatikana katika ufunzaji wa lugha ya pili na usahihi wa ṯafsiri uṯaboreka. Kwa kutumiya harakaṯi walizofanya waṯaalamu wenzet$^h$u kwengineko Afrika Mashariki nasi waṯaalamu wa Kenya tumepawa biri ya kukichangamanisha kiAsiliya katika kiSanifu ili jumuiya nzima ya kiSwahili ifaiḏike. Ṯ$^h$afiṯi zijazo zijaribu kujibu maswali haya: Je, kwa kwingiliwa zaiḏi na jamii ya kiKushiti, ambayo nriyo lugha chanzi ya umenoni (Nurse, 1985), katika miji ya Mkowa wa Pwani ya Kenya, umenoni huu umeengezeka au kupunguwa kwa kiyasi gani katika kiAsiliya? Hili liṯatusaidiya kujuwa kiwango cha hofu ya kiAsiliya. Je, ni vipi uwainaṯi wa lugha uṯatuleteya umoja wa utambulisho wet$^h$u katika jamii ya Kenya, Jumuiya ya Afrika Mashariki na Afrika kwa jumla?

## SHUKURANI

Shukurani zangu za dhaṯi kwa Makamu Mkaṯibu Bw. John Thuku wa Postmordern Library ya KU; Bw. Said Kaonge wa makṯaba ya PU; Profesa R.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.803

Chimerah, na Dkt. A. Taib wa PU; Dkt. A. Roṯich, Dkt. E. Kisurulia, Dkt. S. Sawe woṯʰe wa UoK; na wanafunzi wangu wa Fonetiki na Fonolojiya ambao haweshi kukereka, "kwa nini watufunza sauti zote hiziii?!"

## MAREJELEO

Abdulaziz, M. H. (1979). *Muyaka: 19th century popular poetry*. Kenya Literature Bureau.

Amour, A. K. (2008). Athari za nadharia na kanuni za uandishi wa matamshi ya baadhi ya maneno ya kiSwahili sanifu. Katika N. Ogechi, N. Shitemi, K. I. Simala, (wah.). (2008) *Nadharia katika taaluma ya Kiswahili na lugha za Kiafrika* (uk. 175-184). Moi University Press.

Bakari, M. (1985). The morphophonology of the Kenyan Swahili Dialects. Reimer.

BAKIZA, (2010). *Kamusi la Kiswahili Fasaha*. Oxford University Press.

Barwani, A. M. (1995). *Tarjama ya al muntakhab katika tafsiri ya Qur'ani tukufu*. Dar ul Fajri Islamy.

BBC (2020, November 2). Algorithm spots 'covid cough' inaudible to humans. Imesomwa: https://www.bbc.com/news/technology-54780460

Bigi, B., Péri, P., & Bertrand, R. (2012). Orthographic transcription: Which enrichment is required for phonetization?. The eighth international conference on Language Resources and Evaluation, May 2012, Istanbul, Turkey. pp.1756-1763. hal-00983700

British Library (2020, September 2-3). How Should We Write Yorùbá? A Two-session Online Symposium on Yorùbá Orthography in the 21st Century. Organized by the British Library.

Centre for Advanced Studies of African Society (CASAS), (2012). *A unified orthography for Bantu languages of Kenya*. Monograph no. 249.

Mwita, C. L. (2007). Prenasalization and IPA. *UCLA Working Papers in Phonetics 106*, uk 58-67. Imesomwa: https://escholarship.org/uc/item/9d93t9t9

Chambers, J. K. & Trudgill, P. (2004). *Dialectology* (2nd edition). Cambridge University Press.

Chimerah, R. M. (1999). *Kiswahili past present future horizons*. Nairobi University Press.

Chimerah, R. M. (2020). My recommendations from the Mombasa deliberations. Stakeholders Validation of Languages Bill of Kenya 2015 Conference held at Pride inn Hotel, December 20, 2019.

Chiraghdin, S., & Mnyampala, M. (1977). *Historia ya Kiswahili*. Oxford University Press.

Clements, G. N., & Sylvester O. (2002). Explosives, implosives, and nonexplosives: The linguistic function of air pressure differences in stops. *Laboratory Phonology 7*. Mouton de Gruyter. pp. 299–350.

Crystal, D. (2003). *Language death*. Cambridge University Press.

Eastman, C. M. (1994). Tourism in Kenya and the marginalization of Swahili. Katika Annals of Tourism Research 22 (1), 172-185.

Gekonge, D. (2021, July 3). KICD Invites Applications For Editing 18 Grade 4 Course Books Of Indigenous Languages. Imesomwa: https://teacher.co.ke/kicd-invites-applications-for-editing-18-grade-4-course-books-of-indigenous-languages/ accessed 15/06/2022 9:50 am

Githinji, P., & Njoroge, M. (2017). Folklinguistic perceptions and attitudes towards Kenyan varieties of Swahili. Katika *Swahili Forum 24*, 62-84.

Janson, T. (2007). Bantu spirantisation as an areal change. Katika *Africana Linguistica 13*, 79-116. doi: https://doi.org/10.3406/aflin.2007.972

Hayward, K. M., Omar, Y. A., & Goesche, M. (1989). Dental and alveolar Stops in Kimvita Swahili: An electropalatographic study. Katika *African Languages and Cultures*, *2* (1) 51-72. Imesomwa http://www.jstor.com/stable/1771705

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.803

Karanja, P. N. (2012). Kiswahili dialects endangered: The case of Kiamu and Kimvita. Katika *International Journal of Humanities and Social Science 2* (17), 95-117.

Katz, L., & Frost, R. (1992). The reading process is different for different orthographies: The orthographic depth hypothesis. Katika *Haskins Laboratories Status Report on Speech Research*. SR- 111/112, 147-160.

Kenya National Bureau of Statistics (2009). 2009 Kenya population and housing census: Enumarator's instructions manual. Nairobi.

Khalid, A. (1977). The liberation of Swahili from European appropriation. East africa Literature Bureau.

Krapf, L. (1882). *A dictionary of Suahili language*. Trubner & Co.

Lass, R. (1984). *Phonology: An introduction to basic concepts*. Cambridge University Press.

Lodhi, A. (2003). Aspiration in swahili adjectives and verbs. Katika *Africa and Asia, 3*, 155-160.

Lodhi, A. (h.t). Notes on Swahili phonology. Hazina ya maktaba yake binafsi, Uppsala.

Massamba, D. P. B., Kihore, Y. M., & Msanjila, Y. P. (2004). *Fonolojia ya Kiswahili sanifu (FOKISA) sekondari na vyuo*. TUKI.

Mazrui, A. (2007). Swahili beyond boundaries: Literature, language, and identity. Ohio University Press.

Mazrui, A. M. (1981). *Acceptability in a planned standard: The case of Swahili in Kenya*. Tasnifu ya Uzamifu (Haijachapishwa). Chuwo Kikuu cha Stanford, Stanford.

Mazrui, A., & Chimerah, R. M. (2019). Kuwasilisha ujumbe wa kidini: Baina ya kipwani, kibara na "kipwara". Makala yaliyowasilishwa katika 32nd Swahili Colloquium yenye kauli mbiyu Pwani na Bara Coast and Mainland, Unversitat Bayreuth, Ujarumani.

Mbaabu, I. (1985). New horizons in Kiswahili: A synthesis in developments, research and literature. Kenya literature bureau.

wa Mberia, K. (2016). Mother tongue as media of instruction: The case of Kenya. Katika *The University of Nairobi Journal of Language and Linguistics, 5*, 46-59.

Mgullu, R. S. (1999). Mtalaa wa isimu fonetiki, fonolojia na mofolojia ya Kiswahili. Longhorn Publishers.

Milroy, J. & Milroy, L. (1999). *Authoriy in language: investigating Standard English* (3rd edition). Routledge & Kegan Paul.

Mkude, D. J. (2010). Mtawanyiko wa lahaja za Kiswahili. Katika *Lugha ya Kiswahili*. TUKI (3rd edition), uk. 65-88.

Mose, P. N. (2017). Language-in-education policy in Kenya: Intention, interpretation, implementation. Katika *Nordic Journal of African Studies 26* (3), 215-230.

Munyaya, E. J. (2019, Disemba 19-20). The contribution of KiSwahili in the implemenation of the mother tongue policy: A case study of Kilifi North sub-county, Kilifi County. Iliyowasilishwa katika Kongamano la Kimataifa la KiSwahili, Zanzibar.

Musau, P. M. (1994). Aspects of interphonology: The study of Kenyan learners of Swahili. Bayreuth African Studies.

wa Mutiso, K. (2005). *Utenzi wa Hamziyyah*. TUKI.

Mutambo, A. (2021, October 12). Uhuru at UN: Kenya says identity politics a ticking time bomb. Imesomwa:https://nation.africa/kenya/news/uhuru-at-un-kenya-says-identity-politics-a-ticking-time-bomb-3580204

Nurse, D. (1985). Dentality, areal features, and phonological change in northeastern Bantu. *Studies in African Linguistics*, *16* (3), 243-279.

Nurse, D. & Hinnebusch, T. J. (1993). *Swahili and Sabaki: A linguistic history*. University of California Press.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.803

Olali, T. (2008). An english rendition of a classical Swahili poem. Sahel books Inc.

Polome, E. (1967). *Swahili language handbook*. Center for Applied Linguistics.

Sacleux, C. S. (1939). *Dictionnaire Swahili-Francais*. Institut d' Ethnologie.

Shariff, I. N. (1988). Tungo zetu: Msingi wa mashairi na tungo nyinginezo. The Red Sea Press.

Steere, E. (1919). *A handbook of the Swahili language as spoken at Zanzibar*. Society for Promoting Christian Knowledge.

Stigand, C. H. (1915). A grammar of dialectic changes in the KiSwahili language. Cambridge University Press.

Swaleh, R. H. (2017). *Njeo, hali na dhamira katika kitenzi cha Kitikuu: Mtazamo wa uminimalisti*. Tasnifu ya PhD (haijachapishwa). Pwani University, Kilifi.

Timammy, R. (2002). *Mombasa Swahili women's wedding songs: A stylistic analysis*. Tasnifu ya PhD (Haijachapishwa), University of Nairobi, Nairobi.

TUKI (2013). *Kamusi ya kiswahili sanifu*. Oxford University Press.

UNESCO (h.t) Imesomwa: http://www.ibe.unesco.org/fileadmin/user_upload/Policy_Dialogue/48th_ICE/Press_Kit /Interview_Clementina_Eng13Nov.pdf

University of Cape Town (2022, June 6). KiSwahili as an agent of liberation, integration. Imesomwa: https://www.news.uct.ac.za/article/-2022-06-01-swahili-as-an-agent-of-liberation-integration

Whiteley, W. H. (1993). *Swahili: The rise of a national language*. Gregg Revivals.

Wikipedia.org (2022). https://en.wikipedia.org/wiki/IPA_pulmonic_consonant_chart_with_audio Ilisomwa 15/06/2022 9:00 asubuhi.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.